WIZARA YA AFYA
BARAZA LA FAMASI

MAMBO YA KUZINGATIA ILI KUJIUNGA NA MASOMO YA SHAHADA YA FAMASI

UTANGULIZI

Baraza la Famasi ni taasisi ya Serikali iliyopo chini ya Wizara ya Afya na iliyoanzishwa kwa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Famasi, Sura 311. Pamoja na majukumu mengine Baraza limepewa jukumu la kuhakiki ubora na ujuzi unaotolewa kwa wanataaluma wa kada ya famasi na kuwasajili baada ya kujiridhisha kuwa wanakidhi vigezo vya kuhitimu kutoka vyuo vinavyotambulika.

Kifungu Na.4 (i) cha Sheria kinaeleza kuwa Baraza kushirikiana na mamlaka za ithibati kutafanya tathmini ya viwango vya mafunzo ya kitaaluma vinavyotolewa.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kujiunga na Shahada ya Famasi

Njia mbili (02) za kujiunga;

1.Kujiunga moja kwa moja (Direct entry)

Mhitimu wa kidato cha sita ili kujiunga na shahada ya famasi ni lazima;

(A)

Awe amesoma masomo ya mchepuo wa sayansi kwa Kidato cha nne na Kidato cha sita kwa masomo ya Fizikia, Kemia, Biolojia na Hisabati na kupata alama za ufaulu kwa mujibu wa mwongozo wa Baraza la Taifa la Mitihani (NECTA).

(B)

Awe amesoma mchepuo wa sayansi kwa masomo ya Fizikia, Kemia na Biolojia kutoka kidato cha sita na kupata alama za ufaulu za kujiunga na ngazi ya shahada ya famasi kwa mujibu wa mwongozo wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) wa mwaka husika.

2. Kujiunga kupitia vigezo linganifu (equivalent qualification)

Mhitimu wa ngazi ya Stashahada (diploma) ya famasi ili kujiunga na shahada ya famasi ni lazima;

A) Awe amesoma masomo ya mchepuo wa sayansi kidato cha nne ikijumuisha Fizikia,Kemia,Biolojia, Hisabati na kupata alama za ufaulu za kujiunga na kozi ya famasi ngazi ya kati (NTA L4-6) kwa mujibu wa mwongozo wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) wa mwaka husika.

B) Awe amehitimu mafunzo ya kozi ya famasi ngazi ya diploma (NTA L6) na kupata ufaulu wa kuweza kujiunga na ngazi ya shahada ya famasi kwa mujibu wa mwongozo wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) wa mwaka husika.

Wahitimu wanaosoma shahada ya famasi nje ya Nchi
Wahitimu hawa pia watafuata njia zilizoelezwa hapo juu ikiwa ni pamoja na;

A) Awe amesoma masomo ya mchepuo wa sayansi kwa kidato cha nne na sita au kuhitimu kozi ya famasi ngazi ya Stashahada (diploma) kwa mujibu wa miongozo iliyopo.

B) Awe na cheti cha kumruhusu kusoma elimu ya juu nje ya Nchi kwa shahada ya famasi (No Objection Certificate/NOC) kutoka Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

C)Chuo anachoenda kusoma nje ya Nchi kiwe kinatambuliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Kwa maelekezo zaidi wasiliana nasi kwa barua pepe info@pc.go.tz.

Imetolewa na;
MSAJILI
BARAZA LA FAMASI
S.L.P 1277, Dodoma